TANGAZO LA SERIKALI Na. 807 la Tarehe 01/11/2019.
SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1))

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE ZA MWAKA 2019

Jina na Mwanzo wa Kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Songwe za Mwaka 2019.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Songwe.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma, vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri"maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Songwe;

"Madini ya ujenzi" maana yake ni kokoto, mawe, changarawe, mchanga, chokaa, marumaru, kifusi, udongo mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa katika eneo la Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

Utozaji wa ada na ushuru

4.- (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

Regista katika nyumba za kulala wageni

5. Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni atatakiwa kuandikisha wageni wote katika rejista ya wageni itakayotolewa na Halmashauri baada ya mmiliki wa nyumba ya kulala wageni kulipia ada kwa kiwango kitakachokuwa kimepangwa na Halmashauri.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

6. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

7.- (1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ushuru.

(4) Malipo ya ada na ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama uthibitisho wa malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

8.- (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali

kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake kwa kibali alichopewa na Halmashauri anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa hizo.

(4) Fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(5) Wakala hataruhusiwa kukamata.mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

9.- (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

10. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa na adhabu

11.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi; au

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri au shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa Chini ya Kifungu cha 4(1))

I. ADA YA KUKODISHA MALI ZA HALMASHAURI

Na.	**Huduma**	**Kiwango**
1	Kukodi ukumbi Halmashauri kwa ajili ya mikutano au vikao au sherehe	Kwa mujibu wa mkataba
2	Kukodi viti	Kwa mujibu wa mkataba
3	Kukodi Gari Kukodi trekta	Kwa mujibu wa mkataba Kwa mujibu wa mkataba
4	Vifaa.	Kwa mujibu wa mkataba
5	Kupanga vibanda vya biashara mzunguko wa Stendi na maeneo mengine	Kwa mujibu wa mkataba
6	Vibanda vya biashara sokoni	Kwa mujibu wa mkataba
7	Mali nyingine za Halmashauri	Kwa mujibu wa mkataba

II. ADA NA USHURU WA MAZAO YA CHAKULA NA BIASHARA

Na.	*Zao*	*Kiwango/USHURU*
1	Viazi vitamu	3%ya Bei ya soko
2	Vitunguu maji	3%ya Bei ya soko
3	Matunda	3%ya Bei ya soko
4	Karoti	3%ya Bei ya soko
5	Kabichi	3%ya Bei ya soko
6	Nyanya	3%ya Bei ya soko
7	Maharage	3%ya Bei ya soko
8	Karanga	3%ya Bei ya soko
9	Mchele	3%ya Bei ya soko
10	Mazao ya Mboga Mboga	3%ya Bei ya soko
11	Viazi mviringo	3%ya Bei ya soko
12	Mahindi	3%ya Bei ya soko
13	Uwele	3%ya Bei ya soko
14	Mtama	3%ya Bei ya soko
15	Mpunga	3% ya bei ya soko
16	Mhogo	3%ya Bei ya soko
17	Mazao ya matunda	3%ya Bei ya soko
18	Kahawa	3%ya bei ya soko
19	Vitunguu saumu	3% ya bei ya soko.
20	Ufuta	3% ya bei ya soko
21	Alizeti	3% ya bei ya soko.
22	Mazao mengine	3% ya bei ya soko

III. ADA YA HUDUMA ZA CHANJO, CHAPA, JOSHO, UKAGUZI WA NYAMA NA USHURU WA BUCHA

Na	***Ada/ushuru***	***Kiwango***
1	Ada ya Ukaguzi wa nyama kwa kila Ng'ombe atakayechinjwa	3,000/= kila mmoja
2	Ada ya Ukaguzi wa nyama kwa kila Kondoo, Mbuzi au Nguruwe atakayechinjwa	2,000/= kila mmoja
3	Kuwamba na kukausha ngozi (a) Ng'ombe (b) Mbuzi, Kondoo au mnyama mwingine	 500/= kila ngozi 300/= kwa ngozi
4	Ushuru wa wachoma nyama.	500/= kwa siku.
5	Ada ya uogeshaji mifugo (Josho)	200/= kwa ng`ombe
6	Kibali cha machinjio binafsi	30,000/= kwa mwaka

7	Ada ya kusafirisha ngozi	50,000 kwa mwaka
8	Ada ya chapa ya mifugo.	500 /=
9	Ada ya chanjo ya mifugo	kwa mfugo inategemea bei ya chanjo
10	Ada ya bucha	50,000/= kwa Mwaka

IV. USHURU WA MAUZO YA MIFUGO MINADANI

Na	***Aina ya Mifugo***	***Tozo***
1	Ng'ombe	5,000/= kwa ng'ombe
2	Mbuzi	2,000/= kwa mbuzi
3	Kondoo	2,000/= kwa kondoo
4 5.	Kuku Nguruwe	2,000/= kwa tenga 3,000/= kwa nguruwe
5	Mifugo mingine	2,000/= kila mnyama

V. ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, NA MICHEZO

Na	***A. Ada/Ushuru***	***Kiwango***
1	Leseni ya vibanda vya picha jongevu	60,000/= kwa mwaka
2	Ada ya kumbi kubwaya(watu zaidi 101)	10% ya bei ya tozo.
3	Ada ya kumbi ndogo(watu chini ya 100)	10% ya bei ya tozo.
4	Usajili chama cha Baiskeli	10,000/= kwa usajili.
7	Kibali cha kuchezesha disco, Maonyesho ya bendi, Sanaa za maonyesho (Sinema, video, maigizo, sarakasi, ada nyingine kwa **msanii wa nje ya Halmashauri**.	50,000/= Kwa tukio
8.	Kibali cha kuchezesha disco, maonyesho ya bendi, sanaa za maonyesho (sinema, video, maigizo, sarakasi, ada nyingine kwa **msanii wa ndani ya Halmashauri.**	30,000/= kwa tukio
9	Kibali cha kuchezesha Michezo ya Kubahatisha kwa kutimia mashine.	100,000/= Kwa kibali kwa mwaka
10	Kibali cha mchezo wa pool table	30,000/=kwa mwaka.

VI. ADA NA USHURU WA STENDI NA MAEGESHO KWA MAENEO YALIYOTENGWA

A. MAGARI YA MIZIGO

Aina ya Gari	USHURU		
	Kwa Saa	**Kwa siku**	**Kulaza Gari kwa siku.**
Gari ya Mizigo zaidi ya Tani 5	1,000/=	3,000/=	5,000/=
Gari la Mizigo chini ya Tani 5	500/=	2,000/=	3,000/=
Pick up/Station Wagon	500/=	2,000/=	2,000/=
Lori lenye Trela zaidi ya tani 3	500/=	2,000/=	2,000/=
Lori lenye Trela tani 3 na zaidi	500/=	3,000 /=	4,000/=

B. VYOMBO VYA USAFIRI WA ABIRIA

Na.	Aina ya Chombo	Ushuru(Tshs)
1.	Basi Dogo la abiria kati ya 1 – 20	1,000/= kwa siku
2.	Basi kubwa la abiria kati ya 21 – 30	1,500 /= kwa siku
3.	Basi kubwa la abiria zaidi ya 31	3,000/= kwa siku
4.	Gari Dogo (Taxi Cab)	500/= kwa siku
5.	Gari Dogo (Binafsi)	500/= kwa siku
6.	Magari ya Mizigo (Pick-up)	1,000/= kwa siku
7.	Pikipiki	200/= kwa siku
8.	Bajaji	200/= kwa siku
9.	Magari mengine	1,500/= kwa siku
10.	Ada ya Kuingia stand kwa mtu mmoja asiye na tiketi	200/= kila anapoingia

GHARAMA ZA KUVUTA NA KUHIFADHI CHOMBO CHA USAFIRI KILICHOVUNJA SHERIA

Na.	*Aina ya Chombo*	*Gharama za kuvuta*	*Gharama za kuhifadhi kwa siku*
1.	Basi kubwa la abiria kati ya 20-28	150,000/=	20,000
2.	Basi kubwa la zaidi ya abiria 28	200,000/=	20,000
3.	Basi Dogo la abiria kati ya 1-20	100,000/=	20,000
4.	Gari Dogo (Taxi Cab)	80,000/=	20,000
5.	Gari Dogo (Binafsi)	80,000/=	20,000
6.	Lori na Trela chini ya tani 3	200,000/=	20,000
7.	Lori na Trela tani 3 na zaidi	300,000/=	20,000
8.	Magari ya Mizigo (Pick-up)	80,000/=	20,000
9.	Magari mengine	150,000/=	20,000
10.	Pikipiki na Bajaji	20,000/=	10,000

GHARAMA ZA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI VYA BIASHARA

Na.	*Aina ya Chombo*	*Ada ya usajili kwa mwaka*
1.	Teksi	40,000
2.	Pikipiki	10,000
3.	Bajaji	10,000
4	Boti mita sita hadi mita tisa	60,000
5	Boti chini ya mita sita	45,000
6	Mtumbwi	30,000
7	Jahazi	30,000
8	Ngalawa	30,000
9	Magari ya kukodisha ya binafsi	45,000

VII. USHURU WA MAZAO YA MISITU

Na	Aina ya zao / shughuli	Ushuru (TShs.)
1	Mbao za miti laini ya kupandwa na saizi aina zote	5% ya thamani kulingana na bei ya soko ya ubao .
2	Mbao za miti ya asili na saizi aina zote	5% ya thamani kulinga bei ya soko ya ubao.
3	Nguzo za miti laini na ngumu (softwood & hardwood) zenye kipenyo kati ya 5cm – 10cm	5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko ya nguzo.
4	Nguzo za miti ya laini na ngumu (softwood & hardwood) zenye kipenyo kati ya 10cm – 20cm	5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko ya nguzo.
5	Mkaa kwa gunia la kilo 50	5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko la gunia la mkaa
6	Mkaa kwa gunia la debe 10	5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko gunia la mkaa.
9	Asali	5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko kwa kila lita ya asali.
10	Mazao mengine yasiyo ya mbao	5% kulingana na thamani ya bidhaa kwa bei ya soko.
11	Magogo ya kuni	Tsh 10000/= kwa kila gogo

VIII. ADA YA UPIMAJI WA ARDHI NA VIBALI VYA UJENZI

Na	***A. Ada ya Kibali cha Ujenzi/ Upimaji***	***<u>Kwa kila kibali</u>***
1	Mnara wa simu	500,000/=
2	Jengo la Ghorofa moja	100,000/= kwa kila ghorofa moja
3	Nyumba za Biashara	50,000/=
4	Nyumba ya Makazi	20,000/=

5	Kituo cha mafuta	250,000/=
6	Majengo ya Taasisi Binafsi	150,000/=
7	Maghala na Bohari.	100,000/=
8	Ujenzi wa Uzio	100/= kwa mita za mraba
9	Majengo ya Ibada	100,000/=
10	Vituo vya Utalii/Mapumziko	250,000/=
11	Majengo ya Viwanja	1,000,000/=
12	Viwanda Vidogo Vidogo vya Huduma	200,000/=
13 14 15	Ada ya uchunguzi wa ramani za ujenzi Ada ya ukarabati wa nyumba Maeneo mengine yasiyopimwa ndani ya Halmashauri	10,000/= 15,000/= 10,000/=
Na	***B. Ada ya mabadiliko ya Matumizi ya Jengo***	***Kwa kibali***
1	Nyumba ya kuishi na biashara	40,000/=
2	Nyumba ya Biashara	60,000/=
3	Nyumba ya kuishi	30,000/=
4	Ghorofa	150,000/=
5	Kiwanda, Bohari, Ghala	100,000/=
6	Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Makazi)	20,000/=
7	Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Biashara)	50,000/=
Na.	***B. Ada za huduma ya ardhi***	***Kiwango***
1	Ada ya maombi ya kumilikishwa kiwanja	20,000/= kwa kila ombi.
2	Kutambua eneo (Plot identification)	10,000/= kwa kila plot
3 4	Kurudishia mawe yanaonesha mipaka (Beacon replacement) Ada ya kukagua ramani	6,000/= kwa kila jiwe 20,000/= kwa ramani

IX. USHURU WA HOTEL (Hotel Levy)

Na.	***Aina ya Biashara***	***Kiwango***
1.	Hotel/Nyumba ya kulala wageni	10% ya mauzo kila chumba kwa siku

X. ADA NA USHURU WA HUDUMA NYINGINE

Na.	***Ada***	***Kiwango***
1	Ada ya kupima afya kwa wahudumu wa Baa, Hoteli na Migahawa na maeneo mengine ya kutoa huduma za vyakula au vinywaji kwa umma.	5,000/= kwa kila miezi mitatu (3)
2	Gharama ya kuhifadhi wanyama waliokamatwa kwa kuzurura hovyo kwa siku.	1,000/= kwa ng'ombe 500/= kwa mbuzi 500/= kwa kondoo 1,000/= kwa punda 1,000/= kwa ngamia. 1,000/= kwa mbwa. 1,000/= kwa Nguruwe
3	Faini ya kutovaa sare kwa wahudumu wa Bar, Mgahawa, Hotel na maeneo mengine ya kutoa huduma za vyakula au vinywaji kwa Umma	10,000/= kwa tukio.
4	Ada ya usajili vikundi vya ujasiliamali	25,000/= kwa ombi
5	Ada ya vikundi vya kijamii	20,000/=kwa ombi
6	Ada ya kukagua hesabu za shule za Sekondari Binafsi	100,000/=kwa ombi
7	Ada ya pango la ardhi kwa wamiliki wa maeneo yaliyopangishwa Minara ya Simu	5% ya alicholipwa
8	Mauzo ya vitabu vya stakabadhi za fedha za shule za Serikali.	Bei ya soko.
9	Mauzo ya Hati za Malipo katika vijiji.	Bei ya soko.
10	Mauzo ya vitabu vya hati za malipo shule za Msingi na Sekondari	Bei ya soko.
11	Mauzo ya Vitabu vidogo vya Ushuru mbalimbali	Bei ya soka.
13	Ushuru wa kufanya biashara katika eneo la Halmashauri .	500/= kwa siku

14	Vitabu vya ushuru wa Hotel au nyumba ya kulala wageni	Bei ya soko.
15	Leseni ya Biashara ya Samaki	30,000/=kwa leseni
16	Leseni ya uvuvi	25,000/= kwa mwaka
	Kibali cha kufanya shughuli za uchimbaji madini	100,000/=Kwa mwaka
16	Ushuru wa uchakataji wa bidhaa au mazao(precessing fee)	
17	a. Mchele	500/= kwa gunia.
	b. Mahindi au ngano	1,000 /= kwa tani moja
	Kibali cha kununua mazao ya biashara	200,000/=kwa kibali
17	Kodi ya vibanda kwa watu waliopangisha vyumba vya	
18	biashara.	5% ya kodi ya pango.

XI. ADA YA MAOMBI YA ZABUNI

Na .	***Ombi***	***Kiwango***
1	Zabuni ya ushuru Minada au masoko na mazao	50,000/= kwa kila ombi
2	Zabuni ya kutoa huduma na kazi mbalimbali	50,000/= kwa kila ombi
3	Zabuni ya kazi za ujenzi.	100,000/= kwa kila ombi

XII. USHURU WA MADINI YA UJENZI NA MADINI MENGINE

Na	Aina ya Madini	Kiwango Tsh.
1	Mchanga,Kokoto, mawe, kifusi, tofali	1,000/= kwa tani kwa kila safari
2	Mawe na udongo wa madini/Uchenjuaji	2,500/=kwa tani
3	Madini mengine yeyote	2,000/=kwa tani
4	Ada za uendeshaji viwanda vya kuchakata Madini makarasha	365,000/= kwa mwaka kwa kila karasha
5	Ada ya uendeshaji Plant ya uchenjuaji	1,000,000/=kwa mwaka

XIII. USHURU WA KUFANYA BIASHARA KATIKA MAGULIO AU MINADA AU MASOKO

Na	**Aina Ya Bidhaa**	**Kiwango**
1	Mitumba	500/= kwa siku
2	Vyombo vya nyumbani.	500/= kwa siku
3	Nguo za dukani	500/= kwa siku
4	Samaki,	500/= kwa kilo
5	Urembo	500/= kwa siku
6	Viatu	500/= kwa siku.
7	Biashara nyinginezo.	500/= kwa siku.

XIV. USHURU WA KUSHUSHA MIZIGO KATIKA ENEO LA SOKO LA HALMASHAURI

Na.	Aina ya chombo cha usafiri	Ushuru
1	Uzito wa kuanzia tani 1-5	Tsh.2,000/=
2	Uzito wa kuanzia tani 6-10	Tsh.5,000/=
3	Uzito wa kuanzia tani 11-20	Tsh.10,000/=
4.	Uzito wa kuanzia tani 20-50	Tsh.15,000/=

XV. ADA YA UZOAJI TAKA

ADA ZA UZOAJI TAKA

(i) Viwanda vikubwa/Taasisi…… Sh. 780,000/= kwa mwaka
(ii) Viwanda vidogo ……..Sh. 260,000/= kwa mwaka
(iii) Hoteli……Sh. 180,000/= kwa mwaka
(iv) Mgahawa ……..Sh. 60,000/= kwa mwaka
(v) Duka la jumla ……..Sh. 60,000/= kwa mwaka
(vi) Biashara nyinginezo …….. Sh. 36,000/= kwa mwaka
(vii) Nyumba za kuishi …….. Sh. 18,000/= kwa mwaka
(viii) Masoko/stendi za basi ……..…… Sh. 5,000/= kwa Tani
(ix) Ada ya ushuru wa dampo …… Sh. 5,000/= kwa Tripu

XVI. ADA YA UNYONYAJI WA MAJI MACHAFU KATIKA VYOO KWA KUTUMIA MAGARI YA HALMASHAURI

(i) Maeneo ya biashara ……Sh. 25,000/= kwa kila safari moja na nyongeza ya Sh. 5,000/= kwa kila kilometa moja.

(ii) Maeneo ya makazi ……Sh. 15,000/= kwa kila safari moja na nyongeza ya Shs. 5,000/= kwa kila kilometa moja.

(iii) Nje ya Halmashauri ……Sh. 40,000/= kwa kila safari moja na nyongeza ya Shs. 5,000/= kwa kila kilometa moja.

XVII. ADA YA UPIMAJI AFYA KWA WAHUDUMU WA NYUMBA YA KULALA WAGENI, HOTELI, MGAHAWA, MUUZAJI WA VYAKULA

i. Kupima wahudumu ……..Tsh. 4,000/= kwa kila mtu kwa miezi sita (6).

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa Chini ya Kifungu cha 12)

KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …….. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, kwamba Tarehe …….. ya Mwezi …….Mwaka …….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha …….. cha Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Songwe za Mwaka 2019.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, nipo tayari kulipa kiasi cha shilingi……badala ya kushtakiwa Mahakamani na nipo tayari kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hizo.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe …….. ya Mwezi …… Mwaka ……

Jina ……

Saini ……..……

Mbele ya:

Jina …….. Cheo …….

Saini ……..